

TANZIA

Januari 25,2021



Marehemu Mhandisi Charles Salus Ogare

Mtendaji Mkuu Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka - DART Mhandisi Ronald Lwakatare anasikitika kutangaza kifo cha aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Usafirishaji Mhandisi Charles Salus Ogare kilichotokea saa 11: 00 asubuhi Januari 25, 2021 katika Hospitali ya Mloganzila jijini Dar es Salaam.

Msiba upo nyumbani kwa marehemu Tabata Kinyerezi jirani na Songas jijini Dar es Salaam. Taarifa zaidi za msiba huu ikiwemo taratibu za mazishi zitatolewa baadaye.

Marehemu Ogare alizaliwa Machi 30, 1965, Mkoani Mara.

Mtendaji Mkuu anawaomba watumishi wote kushirikiana katika kipindi hiki kigumu cha msiba.

Bwana Ametoa na Bwana Ametwaa Jina la Bwana Lihimidiwe.